Jina …… **Nambari Yako ……**

Shule ……. **Sahihi ……..**

Tarehe …….

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
(LUGHA)
JULAI / AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA MUUNGANO WILAYA YA BUNGOMA 2010
Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
(LUGHA)
JULAI / AGOSTI 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO:

- Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
- Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani
- Jibu maswali yote.
- Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	JUMLA	

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ni dhahiri shahiri kwamba **uharamia** umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda

©BGM 2010

ya Afrika Mashariki.Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani.Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dar es Salaam mnamo Agosti 7,1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani.Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala-wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingara yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na 'kinyume mbele'. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni.Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utalii kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. ltakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za ***mtandao*** ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyenginezo kwenye kanda ya ***mwambao*** zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

MASWALI

(a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama 3)

…….

…….

…….

…….

…….

…….

(b) Fafanua dhana ya 'kinyume-mbele' kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

…….

…….

…….

©BGM 2010

……

(c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (alama 3)

……

……

……

……

……

……

(d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia (alama 4)

……

……

……

……

……

……

……

……

(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)

(i) uharamia ……

……

(ii) mtandao ……

……

(iii) mwambao ……

……

2. MUHTASARI / UFUPISHO. (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo.

Imesemwa na kurudiwa tena na tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku.Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

©BGM 2010

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

MASWALI

a) Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 – 55) (Alama 6)

Matayarisho

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

Jibu

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

©BGM 2010

……

……

……

……

……

……

……

……

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 55 – 60) (alama6)
Utiririko ni alama 3

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

a) Bainisha mzizi, viambishi awali na tamati katika sentensi hii (alama3)

©BGM 2010

Asihukumiwe.

……

……

……

……

b) Andika kwa umoja (alama2)

Pulikeni wanetu, msicheze na dunia. Mnasikia?

……

……

……

……

c) Andika kwa msemo wa taarifa (alama3)

"Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni, kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho," Maria alimwambia Yusufu.

……

……

……

……

d) Akifisha sentensi hii (alama3)

Oh huu ndio mkutano aliotuitia mmoja wao aliropoka.

……

……

……

……

e) Toa mifano miwili ya; (alama4)

i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo.

……

……

ii) Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo.

……

……

f) Andika sentensi kwa kinyume. (alama1)

Kijakazi aliangika vyombo vya tajiri wake.

……

……

……

g) Mwajiri wao amekuja kuwalipa mshahara. (Andika katika hali ya ukatavu)(alama2)

……

……

……

h) Andika kisawe cha **kielezi** (alama1)

……

©BGM 2010

……

i) Ainisha nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Kikosi cha askari kiliwanasa wezi na kuwarejesha ng'ombe wa maziwa walioibiwa kutoka tarafa ya Kilibwoni.

……

……

……

j) Bainisha kirai katika sentensi hii, na ueleze ni cha aina gani . (alama2)
Kitabu kizuri kimenunuliwa.

……

……

……

k) Iandike sentensi upya kulingana na maagizo
Mwanariadha mmoja tu ndiye aliyefuzu katika mbio hizo
(Tumia hakuna/ila) (alama2)

……

……

……

l) Tumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizoonyeshwa katika sentensi (alama4)
i) Safiri (tendewa) ……..

……

……

ii) -pa (tendeka)……

……

……

m) Eleza matumizi ya 'ku', 'ji' na 'ki' katika sentensi zifuatazo. (alama3)
i) Kuliko na miti hakuna wajenzi ……
ii) Mimi ninajivunia nchi yangu ya Kenya…….
iii) Nikija nitakueleza ……

n) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale (alama4)
Pwaguzi amewaibia wasafiri.

……

……

……

……

……

……

o) Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno **'fuka'**. (alama2)

……

……

……

©BGM 2010

p) Tunga sentensi ukitumia semi **'bwaga zani'** (alama2)

……

……

……

4. ISIMU – JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza majukumu manne yanayotekelezwa na lugha katika jamii (alama4)

……

……

……

……

……

……

……

……

b) Lugha huchangia vipi kuleta;

i) Utengano

ii) Utangamano katika jamii

Utengano (alama 3)

……

……

……

……

……

……

Utangamano (alama 3)

……

……

……

……

……

……

©BGM 2010